

INDA

1. Ni maisha tunaishi, mambo yakenda sambamba,
Kutwa kununa hakwishi, na hasira ikavimba,
Mdomo kutoa moshi, moyo ukashika kamba,
Mambo haya ni aushi, ela bado yanafumba.
2. Kuamba huko pembeni, ili kuteta insia,
Huku ukijifichani, uoneke mzuria,
Huoni haya huoni, wajidhani ni ngamia,
Ambaye hawi tabani, dhiki ikimfikia.
3. Kuteta jambo kusema, si lazima liwe baya,
Japo uyaseme mema, hiyo haitwi hedaya,
Si kanuni kutundama, usidhanie hekaya,
Hili huleta khasama, na watu kukukimbia.
4. Kumbuka maisha moshi , na bidhaa ni mapambo,
Usijidhani aushi, moyo ni kama mtambo,
Mara oye... mara ashi, huyo kapigwa mkumbo,
Hutoka bila tashwishi, hali hujatenda jambo.
5. Kujikwaa kuanguka, si kwamba kuporomoka,
Huweza kututumuka, njia yako ukashika,
Ela kungine hutoka, hadhi ikaporomoka,
Na wa chini huokoka, leo kwake pakapaka.
6. Na hizi hakika kunga, yafaa uzingatie,
Huja zikatoa mwanga, japo sio au sie,
Sio zote ni bananga, kuna moja inga'rie,
Uishike kama panga, tena uing'ang'anie

Hamidu R. Tambwe